

JINA: _____
NAMBARI YA MTAHINIWA: _____
DARASA: _____
SAHIHI: _____
TAREHE: _____

1013/2

P1 KISWAHILI
KARATASI YA PILI
MWIGO WA PTE
MECHI / APRILI 2018
MUDA: SAA 2 ½

MTIHANI WA MWIGO
KARATASI YA PILI
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO

1. Andika jina lako na namba yako kwenye nafasi ulizoachiwa..
2. Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.
3. Mtihani huu una sehemu **Mbili muhimu: FASIHI, na TARATIBU ZA KUFUNDISHA.**
4. Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzoni mwa kila sehemu.
5. Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa.
6. Usitoe karatasi yoyote katika kijitabu hiki.
7. **Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.**

KWA MATUMIZI YA MTAHINIWA PEKEE

| SEHEMU | SWALI | UPEO | ALAMA |
|--------------|-------|------|-------|
| 1 | 1 | 15 | |
| 2 | 2 | 15 | |
| 3 | 3 | 15 | |
| | 4 | 15 | |
| 4 | 5 | 15 | |
| | 6 | 15 | |
| | 7 | 18 | |
| | 8 | 15 | |
| | 9 | 14 | |
| | 10 | 08 | |
| JUMLA | | | |

Kijitabu hiki kina kurasa 21 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

A. SEHEMU YA KWANZA: FASIHI (ALAMA 45)

Jibu maswali mawili tu katika sehemu hii. Lazima ujibu swali la Ushairi na jingine moja kutika Tamthilia au Riwaya.

1. SAID A. MOHAMED. Sikate Tamaa

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Siku moja itafika, katika hii dunia
Itapozuka fanaka, kupotea kwa balia
Haki itakaposhika, batili kuangamia

Uhuru utapoduma, sio ule wa bandia
'Tasitawi mwanadamu, kila atojifanyia
Utakwenda udhalimu, katu hautorejea

Dunia 'tapoamka, itakapoona njia
Hizi shida taondoka, tutaumana kwa nia
Hili jambo la hakika, tarehe meshatwambia

Na hilo jambo karibu, haitimu myaka mia
Itatuishia tabu, waliotusukumia
Yatasibu matulubu, yale tunayowania

Na nyanyaso litapita, kizazi kipyga kungia
Na usawa kitaleta, tena kitashikilia
Na machozi tutafuta maisha mapya huria

MASWALI

- a) Lipe shairi hili kichwa (alama 1)
-
-

- b) Taja mambo matano anayotarajia yafike siku moja duniani (alama 5)

- c) Huku ukitaja mifano, eleza uhuru wa kishairi aliotumia mwandishi (alama 6)

- d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 3)

- i) Balia
-
-
-

ii) Matulubu

iii) Yatasibu

Soma shairi hili kisha ujibu maswali

2. King'ei na Amata: Taaluma ya ushairi

Wakati johari njema, hasa ule wa bahati,
Wakati wenyе neema, mtu huwa ithibati,
Wakati uwe salama, raha hupamba makuti.
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

Wakati ni wa Karima, ndiye mtoa sharti,
Wakati Mungu apima, ye ye Raufu Ladhati,
Wakati ni wa kusema, na kauli ya kaputi,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

Wakati mwana yatima, pato lake ati ati,
Wakati huwa ni chuma, huzikata mifumbati,
Wakati huja adhima, mnyonge kupewa kitii,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

Wakati bahati nyuma, yakuacha katikati,
Wakati una dhuluma, kukutenga kizingiti,
Wakati hauna pima, huja kutatiza tati,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka

Wakati huwa tuhuma, kunyanya ziwa la nyati,
Wakati huo zahama, upitapo na hupiti,
Wakati mwisho nakama, ukayatema matiti,
Wakati titi nyati, hukamuliwa kwa shaka.

Wakati kama mnyama, vyepesi kukusaliti,
Wakati hauna mwema, huja nyuma kama koti,
Wakati tena hukoma, uanguke kama mti,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

Mnyampala M., Diwani ya Mnyapala

- a) Fafanua sifa za wakati kwa mujibu wa shairi (alama 6)
b) Ni nini dhamira ya msanii katika shairi hili? (alama 2)

- c) Taja na utolee mifano tamathali tatu za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 3)

- d) Shairi hili ni la bahari kadha. Zitaje na uzitolee mifano. (alama 4)

TAMTHILIA

JIBU SWALI LA TATU AU NNE

K. W. Wamitila: Pango

3. i) “Lakini ni dua za kuku”
a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)

- b) Taja tamathali moja ya usemi iliyotumiwa katika dondo hili (alama 1)

- ii) “ Suala la ujenzi wa Jamii mpya limeshughulikiwa katika tamthilia ya Pango” Fafanua kwa kutoa mifano mitano (alama 10)

Kithaka wa Mberia: Natali

4. a) Watoto katika Tamthilia ya Natala wamepewa haki mbalimbali. Thibitisha kwa kutoa mifano mitano (alama 10)
b) Baadhi ya wahusika katika Tamthilia ya Natala wamefanya kazi ya wajumbe. Toa mifano mitano na ujumbe walioupeleka (alama 5)

RIWAYA

5. LAMIN H. OMAR: Dunia Mashaka Makuu
“Msiba wa Dunia ulikuwa wa kujitakia”. Jadili (alama 15)
6. J. Habwe: Maisha Kitendawili.
a) “Mui huwa Mwema”.
Kwa kurejelea mhusika Farida, thibitisha kauli hii. (alama 12)

b) Eleza jinsi maombi ya mwombaji wa Dini ya Msalaba Mweusi yalivyomfaa Farida (alama 3)

MBINU ZA KUFUNDISHIA

7. Eleza dhima ya kutumia mchezo wa kuigiza katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili (alama 18)

8. Fafanua jinsi unaweza kufanikisha ziara ya kielimu katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili (alama 15)

9. Unapanga kufundisha uandishi wa Insha kwa jumla katika darasa la saba. Taja mambo muhimu utakayowafundisha wanafunzi wako. (alama 14)
10. Unatarajia kufunza matumizi ya ‘kwa’ katika darasa la saba. Onyesha yale utakayoshughulikia katika uwasilishaji wa mada. (alama 8)